## Kusoma Zaidi

# Insha

**INSHA YA A**

CHUO CHA WALIMU CHA
STASHAHADA CHA ELIMU BORA
S.L.P 220087,
BUKOBA.
20/2/2025.

MHADHIRI WA KISWAHILI,
CHUO CHA WALIMU CHA STASHAHADA
CHA ELIMU BORA,
S.L.P 220087,
BUKOBA.

Kwa Bwana Fakiri,

**KUH: KUOMBA MSAMAHA KWA KUTOHUDHURIA KIPINDI CHA KISWAHILI**

Ninachukua fursa hii kuandika barua hii ili kuomba msamaha kwa kutohudhuria kipindi cha Kiswahili kilichofanyika siku ya Jumatatu. Ninajua kuwa kutokuwepo kwangu darasani kuliathiri maendeleo yangu ya masomo na kuliweza kuleta changamoto kwa ratiba ya darasa.

Sababu ya kutohudhuria kipindi hicho ni kwa sababu nilikuwa na dharura ya kifamilia. Hata hivyo, najua kuwa nilipaswa kukuarifu mapema, na kwa hilo pia naomba msamaha.

Ninaahidi kuwa nitajitahidi kurekebisha hali hii kwa kusoma mada niliyokosa na kuhakikisha sipotezi vipindi vijavyo.

Natumai utakubali ombi langu.

Wako mwaminifu,

*BTele*

Baraka Tele

# Kusoma Zaidi

**INSHA YA B.**

**HARUSI NILIYOHUDHURIA**

Ilikuwa siku ya Jumamosi, nilipohudhuria arusi ya rafiki yangu Hamadi. Hii ilikuwa mojawapo ya harusi zilizopambwa kwa hali ya juu na yenye burudani isiyosahaulika.

Siku ya harusi ilianza kwa maandalizi makubwa. Asubuhi na mapema, tulishuhudia wapishi wakiwa jikoni, wakitayarisha vyakula mbalimbali kama vile pilau, samaki wa kukaanga, na mishikaki. Harufu ya vyakula tamu ilijaa hewani, ikiongeza hamu ya wageni walioanza kufika mapema.

Mchana ulipofika, shughuli kuu ilianza. Bwana harusi alifika akiwa amevalia suti nadhifu ya rangi ya buluu, akipendeza na kuonekana mwenye furaha. Bi. harusi naye alionekana mrembo kama hurulaini akiwa amevalia gauni jeupe lililong'aa chini ya mwanga wa jua. Wageni walipiga vigelegele na kushangilia kwa furaha wakati wawili hawa walipowasili ukumbini.

Shughuli ya ndoa ilifanyika kwa utaratibu mzuri, ikiongozwa na kiongozi wa dini aliyetoa nasaha muhimu kwa wanandoa wapya. Baada ya kiapo cha ndoa, burudani mbalimbali zilifuata kama vile ngoma za asili, muziki wa kisasa, na michezo ya kufurahisha wageni.

Kilichovutia zaidi katika arusi hii ni mshikamano wa watu. Watu kutoka maeneo mbalimbali walikusanyika kusherehekea pamoja, wakionyesha umoja na upendo. Chakula kilikuwa cha kutosha, na kila mtu aliondoka akiwa na tabasamu usoni.

Kwa kweli, arusi hii iliniacha na kumbukumbu za kipekee. Ilikuwa ni siku ya furaha, si kwa maharusi pekee bali kwa kila aliyehudhuria. Ukarimu, burudani, na upendo vilitawala na kutufanya tusahau changamoto za maisha kwa muda. Bila shaka, arusi hii itabaki akilini mwangu kwa miaka mingi ijayo.